## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## TUZO ZA WATOA HUDUMA BORA ZA USAFIRI ARDHINI 2025

*Dar es Salaam, 12 Novemba 2025*

### 1. UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(a) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Sura ya 413, LATRA ina jukumu la kuhamasisha ushindani wenye ufanisi miongoni mwa watoa huduma zinazodhibitiwa. Katika kutekeleza hilo, pamoja na majukumu mengine, LATRA imekuwa ikitoa tuzo kwa watoa huduma bora za Usafiri Ardhini. Kwa mara ya mwisho, LATRA ilitoa tuzo kwa watoa huduma bora na salama mwaka 2024, katika wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani, iliyofanyika Dodoma, ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. Dkt. Philip Isdori Mpango, aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 2. LENGO LA KUTOA TUZO ZA WATOA HUDUMA BORA NA SALAMA

Lengo la tuzo hizo ni kuboresha mazingira ya ushindani wenye tija na ufanisi miongoni mwa watoa huduma, kuchochea uwepo wa mifumo imara na endelevu katika utoaji na upatikanaji wa huduma bora za usafiri ardhini kwa umma kwa kuzingatia **Shabaha za Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDGs 2030).** SDGs 2030 inahamasisha uwepo wa huduma za Usafiri wa umma ulio **Salama, Unaopatikana, Endelevu, wa gharama nafuu, Unaozingatia mahitaji ya makundi maalum, huduma bora kwa wateja**, **Ubunifu na Matumizi ya teknolojia.**

Katika mwaka huu, 2025, LATRA kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta ya Usafiri Ardhini, inaendesha mchakato wa kuwapata watoa huduma bora na salama. Washindi watakaopatikana, watatangazwa na kukabidhiwa Tuzo katika Maadhimisho ya Kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini 2025 yanayotarajiwa kufanyika Nchini, Jumatatu tarehe 24 hadi Jumamosi, tarehe 29 Novemba 2025, katika viwanja vya

Mnazi Mmoja (Maonesho ya Shughuli za Usafiri Ardhini) na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (Mikutano ya Kutoa Elimu), Dar es Salaam.

## 3. MAKUNDI YA WATOA HUDUMA NA VIGEZO VYA KUPATA WASHINDI

### 3.1. Makundi ya Washiriki

Washiriki wa tuzo hizo wamegawanywa katika **makundi 08** kulingana na huduma wanazotoa katika sekta ya Usafiri Ardhini ambao ni;

1) Watoa Huduma kwa Mabasi ya mikoani na nchi jirani,
2) Watoa Huduma kwa Magari ya Mizigo,
3) Watoa Huduma kwa Magari Maalum ya Kukodi (Special Hire)
4) Madereva na Wahudumu wa Mabasi ya mikoani na nchi jirani,
5) Watoa Huduma kwa Mifumo ya Tiketi Mtandao,
6) Watoa Huduma za Mifumo ya Teksi Mtandao,
7) Watoa Huduma za Kufunga Vifaa vya Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD), na
8) Waandishi wa Habari na Vyombo vya Habari vilivyoandika taarifa za Sekta ya Uchukuzi.

### 3.2. Vigezo vya Kupata Washindi

Vigezo vinavyotumika kupata washindi vinajumuisha maeneo yafuatayo,

1) Usimamizi wa Vyombo vya Usafiri
2) Usimamizi wa Huduma za Usafirishaji
3) Usimamizi wa Wafanyakazi wa Kampuni/Mtoa Huduma
4) Uhakika wa Huduma za Kampuni/Mtoa Huduma
5) Usalama na Ubora wa Huduma kwa Wateja
6) Ubunifu na Matumizi Sahihi ya Teknolojia
7) Huduma Endelevu kwa Kipindi Chote cha Mwaka wa Tathmini
8) Utii wa Sheria na Kanuni za LATRA na Usalama Barabarani
9) Utunzaji wa Mazingira
10) Kutumia Madereva Waliothibitishwa na Wahudumu waliosajiliwa LATRA

## 4. WATOA HUDUMA WALIOKIDHI VIGEZO VYA AWALI

LATRA kwa kushirikiana na Kamati ya Tathmini ya Awali ya Watoa Huduma Bora na Salama – 2025 imekamilisha mchakato wa awali na kupata Watoa Huduma waliokidhi viwango vya kuingia kwenye Mchakato wa Mwisho wa kupat a Washindi. Makundi hayo na Watoa Huduma husika ni kama ifuatavyo:

### 1) Watoa Huduma kwa Mabasi ya Mikoani na Nchi Jirani

Watoa Huduma 37 kwa Mabasi yaendayo Mikoani na Nchi Jirani waliokidhi vigezo vya awali ni kama ifuatavyo;

#### A. WASAFIRISHAJI WAKUBWA (Mabasi zaidi ya 30) - 07

1) NEW FORCE ENTERPRISES LTD (NEWFORCE)
2) BM ONE COACH LIMITED (BM)
3) ISSA KASSIMU NKYA (HAPPY NATION)
4) AHMED MABKHUT SHABIBY (SHABIBY LINE)
5) SAID MOHAMED & BROTHERS COMPANY LIMITED(NYEHUNGE)
6) YAHAYA ALLY AMOUR (ALLY'S STAR)
7) ABOOD BUS SERVICE LIMITED(ABOOD)

#### B. WASAFIRISHAJI WA KATI (Mabasi 11 hadi 30) - 15

1) SAID MABKHUT SAID (SATCO)
2) HAI TRAVELERS COMPANY LIMITED (HAI)
3) OMARY MARCUS MSIGWA (SUPER FEO)
4) LUCY PANTALEO NJAU (MAPENZI YA MUNGU)
5) HAMAD KHALFAN SUDI (ADVENTURE)
6) VICENT INNOCENT AMANI (ASANTE RABI)
7) TAHMEED COACH TZ LIMITED(TAHMEED)
8) DASTAN HINJU KISUMAPAI (KISUMAPAI EXPRESS)
9) ESTHER LUXURY COACH LIMITED
10) KILIMANJARO TRUCK COMPANY LIMITED (KILIMANJARO EXPRESS)
11) SALUM MIKIDADI HAMISI (TAKBIR)
12) TASHRIFF TRANS

13) TILISHO COMPANY LIMITED (TILISHO)
14) ZBJ ENTERPRISES CO.LTD (BUTI LA ZUNGU)
15) KISIRE TRANS LIMITED

**C. WASAFIRISHAJI WADOGO (Mabasi 4 hadi 10) - 15**

1) RAQEEB TRANSPORT COMPANY LIMITED(RAQEEB)
2) KAIZIREGE ENGLISH MEDIUM BOARDING SCHOOL LTD(KAIZIREGE)
3) RASHID SAID KHALIFA (KSK)
4) KULWA BUNALA MASHIMBA (MASHIMBA EXPRESS)
5) JACOB DUKA MALESA (MALLESAS COACH)
6) AGNESS LINUS KABELEGE (NJOMBE EXPRESS)
7) IDD HAMIS JUMA (RUCHORO)
8) HATIBU ALLY MBERESERO (KIBO)
9) NURUDIN SALIM KILUA (KILUWA EXPRESS)
10) ERFRA GENERAL COMPANY LIMITED
11) MANING NICE CO.LTD
12) MOHAMED SAID MSUYA (LAVIHA)
13) SEIF OMARY LUWINZO (LUWINZO)
14) MARANGU BUSINESS SERVICES LIMITED
15) JUMA MOHAMED ATHUMANI (GREEN LINE)

**2) Watoa Huduma kwa Magari ya Mizigo**

Watoa Huduma 51 kwa Magari ya Mizigo waliokidhi vigezo vya awali ni kama ifuatavyo;

**A. KUNDI A (Magari zaidi ya 1,000) - 06**

1) SPECIALISED HAULIER (T) LTD
2) E. AWADH & CO. LIMITED
3) USANGU LOGISTICS (T) LIMITED
4) AL HUSHOOM INVESTMENT (T) LTD
5) GALCO LIMITED
6) BAKHRESA FOOD PRODUCTS LTD

**B. KUNDI B (Magari 501 hadi 1,000) - 15**

1) GSMHQ HAULAGE LIMITED
2) AM-PM LIMITED
3) TANZANIA ROAD HAULAGE (1980) LIMITED
4) MIGHTY LOGISTICS LIMITED
5) BLUE COAST INVESTMENT LIMITED
6) TAHMEED COACH TZ LIMITED
7) SUPERSTAR FORWARDERS COMPANY LIMITED
8) RAS LOGISTICS (T) LTD
9) ASAS TRANSPORTERS CO LTD
10) A.K TRANSPORT COMPANY LIMITED
11) INARA INVESTMENTS (T) LIMITED
12) IMPERIAL ROAD HAULAGE LIMITED
13) TRANSCARGO LIMITED
14) MOHAMOOD MOHAMED DUALE TRANSPORTER LTD
15) SAID SALIM BAKHRESA & COMPANY LIMITED

**C. KUNDI C (Magari 101 hadi 500) - 15**

1) ITRACOM FERTILIZERS LIMITED
2) BARWAAQO INVESTMENTS LIMITED
3) MANSOOR INDUSTRIES LIMITED
4) GSG ENERGIES TRANS LIMITED
5) ICHEETAH LOGTECH TANZANIA LIMITED
6) TRANSCONNECT LOGISTISC T LTD
7) MARIAM HAULIERS COMPANY LIMITED
8) AFRICA WAKAWAKA LOGISTICS CO. LIMITED
9) ZJBT INVESTMENT LIMITED
10) D & M TRANSPORTER LIMITED
11) ZAMZAM ROAD HAULAGE LTD
12) ELVETH LOGISTICS LIMITED
13) JAH PEOPLE INVESTMENT TRANSPORT COMPANY LIMITED
14) RAM LOGISTICS LIMITED
15) TRANSCARGO LIMITED

D. **KUNDI D (Magari 50 hadi 100) - 15**

1) AFROIL INVESTMENT LIMITED
2) BARREL HAULAGE CO. LTD
3) NOVA ESPERANCA SERVICES LIMITED
4) ARNOLD BENJAMIN LEMA
5) INTERTZ LOGISTICS COMPANY LIMITED
6) TRISTAR ENERGY(TANZANIA) LIMITED
7) ALLYEN LOGISTICS LIMITED
8) SINOMACARGO INTERNATIONAL NIGERIA LTD
9) HGC TRANSPORT & LOGISTICS LIMITED
10) TRANSCARE LOGISTICS LIMITED
11) JMR TRUCKING LIMITED
12) JAMBO & SONS TRADERS COMPANY LIMITED
13) NLCOM (TZ) LIMITED
14) 313 HAULIERS LIMITED
15) PMR ROADWAYS LIMITED

**3) Watoa Huduma kwa Magari Maalum ya Kukodi (Special Hire) - 3**

Watoa Huduma 03 wa Magari Maalum ya Kukodi waliokidhi vigezo vya awali ni hawa wafuatao:

1) FRANK NDEKARISHO MMBANDO
2) SUFIAN SHAIBU MGUDE
3) FINA AMBROSI MAKOI

**4) Watoa Huduma Mifumo wa Teksi Mtandao (Ride Hailing Platform) - 12**

Watoa Huduma 12 wa Mifumo wa Teksi Mtandao waliokidhi vigezo vya awali ni hawa wafuatao:

1) Binary Ethos Company Limited
2) FARAS Technologies Co Ltd-FARAS
3) Uber Tanzania
4) Bolt Tanzania Limited
5) T-Smart African Tours Limited - T Ride

6) Kensrin Company limited
7) Twende Technologies Ltd
8) Safiri Tanzania Limited
9) Tanzania Post Corporation- SwifPark
10) Mswahili (T) Limited– Bantu
11) GOZIDI LIMITED
12) Tanzania App System (Indrive)

**5) Watoa Huduma Mifumo wa Tiketi Mtandao - 05**

Watoa Huduma 05 wa Mifumo wa Tiketi Mtandao waliokidhi vigezo vya awali ni hawa wafuatao:

1) WEB CORPORATION TANZANIA LIMITED
2) OTAPP AGENCY COMPANY LIMITED
3) HASHTECH TANZANIA LIMITED
4) BUSBORA COMPANY LIMITED
5) IYISHE COMPANY LTD

**6) Watoa Huduma wa Kufunga Vifaa vya Kufuatilia Mwenendo wa Magari - 04**

Watoa Huduma 04 wa Kufunga Vifaa vya Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD Vendors) waliokidhi vigezo vya awali ni hawa wafuatao:

1) TERA TECHNOLOGIES
2) ICTPACK SOLUTION
3) EASY TRACK
4) FLEET TRACK

**7) Madereva na Wahudumu wa Mabasi Yaendayo Mikoani na Nchi Jirani**

Abiria wanaosafiri kwenye mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani watapata fursa ya kuwapigia kura madereva na wahudumu (makondakta) waliosafiri nao kwa kujaza dodoso kwa njia ya mtandao (**eDodoso**) zilizoandaliwa zenye lengo la kupima kiwango cha ubora wa huduma walizotoa kwa wateja wao.

Dereva na Mhudumu watapaswa kuwatangazia abiria Namba ya Basi, Jina la Kampuni/Basi, majina yao Kamili na Namba za Leseni (Dereva) / Namba ya

Kusajiliwa LATRA (Mhudumu). Pia kuwajulisha na kuomba kupigiwa kura kupitia mtandao kwa eDodoso kama wanaridhishwa na huduma za usafiri huo.

Washindi watakuwa miongoni mwa Madereva watakaopata kura nyingi na wawe ni wale waliothibitishwa na Mamlaka.

**8) Waandishi wa habari na Vyombo vya Habari**

Vigezo vya Tuzo kwa waandishi wa habari ni kama ifuatavyo:

1. Mwandishi awe anatambulika na Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari
2. Kazi iwe imechapishwa kati ya tarehe mosi Julai 2024 hadi 30 Juni 2025,
3. Kazi iwe imezingatia umahiri wa uandishi wa habari
4. Kazi imechapishwa katika gazeti, chombo cha habari cha kieletroni au kidijiti
5. Kazi imezingatia mizani ya uandishi wa habari za usafirishaji
6. Kazi ziwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza

Vigezo vya Tuzo kwa vyombo vya habari

1. Idadi ya habari zilizofanya vizuri kupitia waandishi wao (Na. Mwandishi wetu inakubalika)
2. Kuwa na vipindi vinavyohusu usafirishaji vinavyozingatia mizani ya uandishi wa habari

Kazi hizo zitumwe kupitia baruapepe info@latra.go.tz au WhatsApp namba 0681 300 800 au mfumo wa edodoso kupitia madodoso yatakayotolewa na LATRA katika tovuti ya LATRA na mitandao ya kijamii

## 5. UTARATIBU WA KUPIGA KURA

Kupitia vigezo vilivyowekwa, watumiaji huduma, na wadau wa usafiri ardhini watapata fursa ya kushiriki kwa kuwapigia kura watoa huduma bora za Usafiri Ardhini kwa kujaza dodoso linalopatikana kwenye tovuti ya LATRA www.latra.go.tz, tovuti ya Maadhimisho www.tanzaniatransportweek.co.tz, eDodoso na mitandao ya kijamii.

## 6. MWISHO WA KUPIGA KURA

Siku ya mwisho ya kupiga na kutuma habari ni siku ya Alhamisi tarehe 20 Novemba 2025.

7. **WITO KWA WADAU**

Tunatoa wito kwa wadau wote kushiriki katika Maadhimisho ya Kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini kupitia Maonesho yatakayofanyika viwanja vya Mnazi Mmoja tarehe 24 hadi 29 Novemba na Mikutano itakayofanyika tarehe 25 hadi 27 Novemba 2025 Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) ili kunufaika na maadhimisho hayo.

Digitally Signed By Salum PAZZY
Wed Nov 12 15:30:00 EAT 2025

Salum PAZZY
**Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**

**TAREHE 12 NOVEMBA, 2025**